# MWONGOZO KUHUSU VIGEZO NA SIFA ZA KUTEULIWA KWA WAKUU WA IDARA YA AFYA NA WASIMAMIZI WA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA MATIBABU (KINGA/TIBA) KWENYE NGAZI ZA SERIKALI ZA MITAA

## 1.0 UTANGULIZI

Sera ya Afya 2007, Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya - 3 (HSSP III) 2009, Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) 2007, Mabadiliko katika mifumo na utoaji wa huduma kwa sekta ya Afya (Health Sector Reform) na pia mabadiliko katika mifumo ya utoaji huduma na uletaji maendeleo kwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Local Government Reforms), viliainisha uwepo wa ofisi ya Mkuu wa Idara ya Afya katika Halmashauri na timu ya uendeshaji wa huduma za Afya (D/CHMT), Bodi ya Afya ya Wilaya (CHSB-Council Health Service Board) ili kuweka mifumo ya; kuinua viwango vya Afya kwa Jamii, (Health Promotion), kuweka mifumo ya kutoa huduma za kinga na tiba ya magonjwa (Disease Prevention), and (Curative/treatment of Diseases) na utengamao (Rehabilitation).

1.1 Idara ya Afya ni miongoni mwa Idara zilizopo katika **Mamlaka za Serikali za Mitaa**, yenye jukumu la kuhakikisha kuwa **huduma za afya zinatolewa** kwa kiwango kilichokusudiwa, kwa mujibu wa mgawanyiko wa majukumu mbalimbali ya uendeshaji wa huduma za Afya, kwa ngazi ya **Mkoa, Halmashauri, Kata, Kijiji na Kaya,** kama inavyoelekezwa na Sheria na Miongozo ya Sekta ya Afya, inayosimamiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

1.2 **Mkuu wa Idara ya Afya** katika Mamlaka za serikali za Mitaa, kulingana na **Sheria na Miongozo ya kisekta,** anaitwa **Mganga Mkuu wa Wilaya, Mji, Manispaa au Jiji.** Licha ya kuwa na uzito sawa na Wakuu wengine, majukumu ya Mkuu huyu kwa baadhi ya maeneo, hutofautiana kutokana na **jiografia ya eneo,** kwa mfano, maeneo ya **Majiji, Manispaa, Miji, Wilaya - Vijijini na Mipakani.** Vilevile hutegemeana na utofauti katika **viashiria vya Afya bora,**



Scanned by CamScanner

kunakosababishwa na mwenendo wa maambukizi, kwa magonjwa ya kuambukiza na kulingana na hali halisi kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Majukumu hayo ni kama ifuatavyo:

i) Kumshauri Mkurugenzi, katika masuala yote ya Afya katika Wilaya/Halmashauri;
ii) Kuwa Msimamizi Mkuu wa masuala yote ya kitaalamu ya afya, kuanzia ngazi ya Wilaya/Halmashauri mpaka kwenye jamii.
iii) Kuongoza timu ya usimamizi wa huduma za afya ndani ya Wilaya/Halmashauri (CHMT).
iv) Kusimamia na kuhakikisha huduma bora za afya ikiwemo matibabu kwa wagonjwa, zinapatikana katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya ndani ya Wilaya, kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya hadi hospitali za Wilaya.
v) Kuandaa taarifa zote za Afya za Wilaya/Halmashauri.
vi) Msimamizi Mkuu wa Rasilimali watu, fedha, vifaa, majengo na dawa katika Halmashauri na ngazi zote za vituo vya kutolea huduma za afya ;
vii) Kusimamia na kushauri katika kuandaa na utekelezaji wa mipango ya Afya ya Wilaya/Halmashauri, kwa kushirikiana na Viongozi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati pamoja na wadau mbalimbali.

1.3 Kati ya mwaka 2005 hadi sasa, kumekuwa na ongezeko kubwa la Madaktari wenye Shahada ya Kwanza (Medical Doctors - MD) na Shahada ya Uzamili katika Afya ya Jamii (Masters in Public Health - MPH) na Shahada ya Uzamili katika Utibabu (Clinical Specialist - Masters in Medical Specialities - MMed) kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na Utumishi wa Umma kwa ujumla. Hali hiyo imesababisha kuwako na umuhimu wa kuangalia upya mgawanyo wa majukumu, kulingana na sifa na uwezo wa rasilimali watu iliyopo sasa katika sekta ya Afya, hasa katika uongozi wa ngazi ya Mkuu wa Idara ya Afya na Wasaidizi wa Mkuu wa Idara, na pia, Wasimamizi wa Hospitali za Wilaya/Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati.



Scanned by CamScanner

## 2.0 SIFA ZA MKUU WA IDARA YA AFYA

Kulingana na mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa Huduma za Afya nchini **(Health Services Scheme - 2009), Ikama ya watumishi wa Afya ya mwaka 2014-19, (Staffing Levels of Public Health Facilities 2014-19)**, na upana wa maeneo yanayoguswa na taaluma za sekta ya afya, ambazo ni; **Uboreshaji Afya, Kinga na Tiba ya Magonjwa na Utengamao,** kama inavyoainishwa katika **Sera ya Afya ya 2007, MMAM 2007** na **Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya - 3 (2009)** na **Na. 4 (2015),** sifa hizo zimepangwa kwenye sehemu mbili, kuonesha hali halisi ya maendeleo hayo:

### 2.1 Sifa za Awali

Kwa mujibu wa Waraka wa Katibu Mkuu, OR - MUU, Kumb Na. C/CB/271/431/01/F/23, wa tarehe 02/01/2005, Wakuu wa Idara ya Afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaitwa Waganga Wakuu wa Wilaya (District Medical Officers), wanapaswa kuteuliwa baada ya kuwa na sifa zifuatazo:

i) Kuwa na elimu ya shahada ya kwanza katika fani ya Udaktari/Afya ya Mazingira/wadudu au uongozi wa huduma za afya;

ii) Kuwa na uzoefu wa miaka minne kazini katika cheo cha udaktari na uzoefu wa miaka saba kwa wataalamu wenye shahada ya Afya mazingira au uongozi wa huduma za Afya;

iii) Kuwa na maadili na sifa za kiusalama za kumwezesha kumudu cheo cha uongozi kufuatia matokeo ya upekuzi.

2.1.1 Vigezo tajwa hapo juu, vimekuwa vikitumika kuanzia mwaka 2005, hadi sasa. Kwa kiasi kikubwa vimewezesha kupata wakuu wa Idara wenye sifa ya Shahada ya Udaktari na uzoefu wa miaka minne. Hata hivyo, katika kufikia malengo ya sera na mikakati ya



Scanned by CamScanner

Afya, hususani; **Maboresho ya Huduma za Uinuaji wa Viwango vya Afya, (Promotive Halth Services), Kinga na Tiba ya Magonjwa yanayoambukizwa na siyo ambukiza (Preventive and Curative Health Services), Utengemao (Rehabilitative Health Services), ikijumuisha** *huduma za Hospitali, ambako kuna mahitaji ya taaluma ya utibabu*, kumekuwa na changamoto katika utekelezaji. Pia, ikizingatiwa hali ya sasa, ambapo *uzalishaji wa Madaktari umeongezeka kwa idadi*, na suala la kujiendeleza limebadilika na *kuongeza aina ya Madaktari wenye Shahada za Uzamili katika fani za Afya ya Jamii na Utibabu ngazi ya Ubingwa* **(Clinical Specialities)** *wameongezeka kwa Idadi na Ujuzi wao, imelazimu kupitia upya vigezo hivyo, ili viendane na Matakwa ya Taaluma, Sera ya Afya, Sheria za Utoaji Huduma, Mipango Mikakati na Program zilizopo.*

**2.1.2** Hali hii imeonesha umuhimu wa kuhuisha sifa za uteuzi, na kisha kupanga upya safu ya **Wakuu wa Idara katika Mikoa na Halmashauri**, na pia, **Wasimamizi wa Hospitali za Rufaa Mikoa, Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati**, kwa nia ya kuboresha huduma na usimamizi wa Sekta ya Afya, katika ngazi zote za Mikoa na Halmashauri.

**2.2 Sifa za Sasa na vigezo vya uteuzi**

Mkuu wa Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii (District Medical Officer), apatikane baada ya kuwa na sifa na vigezo vifuatavyo;

i) **Shahada ya kwanza ya Udaktari (Medical Doctor - MD) - kama taaluma, sera na sheria zinavyoelekeza, na Shahada ya Uzamili katika Afya ya Jamii (Masters in Public Health - MPH) au shahada ya uzamili katika fani za (Health Economics, International Health, Tropical n.k.)** na **uzoefu** wa kazi katika fani ya **udaktari kwa zaidi ya miaka minne.**

ii) Daktari mwenye **shahada ya kwanza (MD) na uzoefu wa miaka minne au zaidi**, ambaye hana shahada ya



Scanned by CamScanner

uzamili katika **afya ya Jamii (MPH)** anaweza kuteuliwa kushika wadhifa wa *Mganga Mkuu wa Wilaya kwa masharti ya kujiendeleza kwa kujiunga na masomo ya shahada ya uzamili katika afya ya Jamii* na kufaulu ndani ya *miaka miwili.* Sifa hii itatumika pale tu ambapo imeonekana hakuna Daktari mwenye sifa tajwa katika Kipengele na (i).

iii) **Daktari Mwenye Shahada ya Uzamili, (Masters in Medical or Surgical Specialities) eneo la Utibabu (Clinical Care)**, atatakiwa kuhamia **Hospitali ya Rufaa Mkoa au Kanda,** kulingana na vigezo vya Ikama hiyo ya 2014/2019, kutoa huduma za *Ubingwa (Specialists Care).*

iv) **Daktari mwenye Shahada ya Kwanza ya Udaktari wa Upasuaji Meno (DDS)** atakuwa **Msimamizi Mkuu wa Huduma za Afya ya Kinywa na Meno, na Msaidizi Mkuu wa Mkuu wa Idara ya Afya kwenye Halmashauri, na pia kwenye Hospitali ya Halmashari, kama taaluma, Sera, Sheria za Utoaji Huduma za Afya, Mipango Mikakati na Program, zinavyoelekeza.**

## 3.0 MGANGA MKUU WA HOSPITALI YA WILAYA/ HALMASHAURI, VITUO VYA AFYA NA ZAHANATI;

Sambamba na utekelezaji wa maboresho ya mifumo ya uendeshaji wa huduma za Afya, pia ulianzishwa uboreshaji wa huduma za Hospitali (Hospital Reforms), kwa ngazi za Taifa, Kanda, Mikoa na Halmashauri, kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za afya katika Hospitali na kuhakikisha unakuwepo uongozi/manejimenti ya Hospitali na Wilaya/Halmashauri kwa ujumla. Katika kutekeleza maboresho hayo ni muhimu sana kuhakikisha kuwa Wilaya/Halmashauri zinakuwa na kiongozi mwenye sifa zilizoainishwa (Mganga Mkuu wa Wilaya/Halmashauri) pamoja na waganga wafawidhi wa Hospitali za Wilaya/Halmashauri, hadi ngazi ya vituo vya afya na Zahanati.



Scanned by CamScanner

**3.1 Majukumu ya Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya/ Halmashauri**

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya/Halmashauri ana jukumu la kusimamia uendeshaji wa Hospitali kwa kutumia **Timu ya Utendaji ya Hospitali (Hospital Management Team - HMT)** chini ya uongozi wa **Kamati ya Uongozi wa Hospitali (Council Hospital Governing Committee - HGC).**

**3.2 Sifa za Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya/Halmashauri;**

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya/Halmashauri ateuliwe baada ya kuwa na sifa zifuatazo;

i) Daktari mwenye **shahada ya kwanza ya Udaktari (MD)** na awe amefanya **kazi za utibabu katika hospitali ya Wilaya sio chini ya miaka mitatu**

**AU**

ii) **Daktari Msaidizi (AMO)** mwenye **uzoefu wa zaidi ya miaka mitatu na mwenye shahada ya uzamili katika afya ya Jamii (MPH).**

iii) **Daktari mwenye Shahada ya Kwanza ya Udaktari wa Upasuaji Meno (DDS)** atakuwa msimamizi Mkuu wa Huduma za Afya ya Kinywa a Meno, na Msaidizi wa Mganga Mkuu

**3.3 Sifa za Wakuu wa Vituo vya Afya**

Vituo vya Afya ngazi ya Kata, vitakua chini ya Mkuu wa Kituo, ambaye ni **Daktari Msaidizi (AMO)**, mwenye uzoefu wa **mwaka mmoja au zaidi,** atakaeongoza kwa kutumia **Timu ya Menejimenti ya Kituo cha Afya (Health Centre Management Committee – HCMC)** na kwa usimamizi wa **Kamati ya Afya ya Usimamizi wa Kituo cha Afya (Health Facility Committee – Health Centre).**

**3.4 Sifa za Wakuu wa Zahanati**

Zahanati ngazi ya Kijiji, itakuwa chini ya Mkuu wa Zanahati, ambaye ni; **Tabibu (Clinical Officer/CO), mwenye uzoefu wa mwaka mmoja au zaidi, atakaeongoza kwa kutumia Timu ya Menejimenti ya Zahanati, (Dispensary Management**



Scanned by CamScanner

**Committee - DMC)** na **Kamati ya Afya ya Usimamizi wa Zahanati (Health Facility Committee - Dispensary)**.

## 4.0 HITIMISHO

Pamoja na sifa zilizoainishwa, **utaratibu wa upekuzi utaendelea** kuwa kigezo kikuu cha **kuthibitisha sifa za maadili.** Maelekezo ya vigezo na sifa zilizoainishwa, yanawasilishwa ili **kuziwezesha Halmashauri kuwa na wakuu wa Idara ya Afya na wasimamizi wa vituo vya Tiba, wenye sifa** kutokana na watumishi waliopo katika utumishi wa Umma, **kwa nia ya kuboresha huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.**



Scanned by CamScanner